# Mwanamke Dhidi ya Uanauke Wake katika Karne ya 21

*Davian Buguna*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Nafasi ya watunzi wa ushairi wanawake, katika ushairi wa Kiswahili inaendelea kukua kwa kiasi kikubwa. Mwanamke baada ya kuchorwa katika kazi mbalimbali za kifashi kwa mtazamo duni na watunzi wa kiume anawajibu wa kujitetea yeye mwenyewe. Makala haya yanalenga kutathmini mtazamo wa mshairi mwanamke juu ya mambo mbalimbali yanayomzunguka mwanamke katika maisha yake ya kila siku. Data za makala haya zilipatikana katika diwani ya Kurunzi ya mwandishi Rose Mbijima kwa mbinu ya usomaji makini. Matokeo yanaonesha kuwa mwanamke anapiga hatua kujiodoa kuwa mtu wa hadhi ya chini, kama ambavyo anachorwa katika kazi nyingi za kifasihi. Hata hivvyo, data zinaonesha kuwa Mwandishi Rose Mbijima anaendelea kumchora mwanamke kwa mtazamo hasi na wakimapokeo zaidi kuliko alivyomfunua kwa matazamo wa kisasa na chaya. Data zinadhihirisha kuwa yapo mambo kuhusu mapenzi na ndoa ambayo mtunzi anamtazamo wa kimapokeo kama zilivyo jamii nyingi za kiafrika. Aidha, kuhusu mtazamo chanya na wakimapinduzi juu ya mambo mbalimbali yanayoendelea katika jamii yake, mwanamke ameonekana akipaza sauti na kutoa maoni yake. Makala haya, yanahitimisha kwa kutoa mapendekezo kuwa, watunzi wa kike wa ushairi wapewe majukwaa mengi zaidi ili waweze kuwasilisha kazi zao, hali ambayo itaendelea kuchochea mabadiliko makubwa ya wanawake juu ya mtazamo wao kuhusu uanauke wao na jamii kwa ujumla kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.**

**Maneno Muhimu:** *Mwanamke, Nafasi ya Mwanamke, Ushairi, Mtazamo wa Kimapokeo, Mtazamo wa Kisasa*

## Utangulizi

Nafasi ya mwanamke katika kazi za fasihi imelezwa kwa mtazamo unaodhaniwa kuwa ni hasi na watunzi na wahakiki mbalimbali wa kazi za kifasihi (Ngaiza, 2004). Wanawake wanaona kuwa wamesawiriwa katika kazi nyingi za kifasihi kwa mtazamo duni sana ukilinganisha na mwanaume (Lyatuu, 2011). Mwanafasihi Indede (2011), anasema Jambo la kushangaza ambalo linaleta ugumu katika kujadili nafasi ya mwanamke kwa mtazamo mpana zaidi ni kuwa ushairi ambao umeandikwa na wanawake ni nadra sana na hasa katika enzi ya karne ya ishirini na moja. Hivyo, kazi nyingi za ushairi ambazo zinatumika kuhakiki suala la nafasi ya mwanamke ni zile ambazo zimeandikwa na wanaume. Mawazo haya yanadhihirisha kuwa swala la nafasi ya mwanamke katika jamii halijatendewa haki katika kujadiliwa kwa kukosekana kwa usawa wa kimtazamo kati ya watunzi wa kiume na wa kike wa ushairi.

Aidha, Mwakanjuki (2022) anaeleza kuwa wahakiki wengi wa fasihi za Kiafrika wanakumbana na wanawake katika miktadha mingi, lakini wanakwepa kuhakiki uhusika wao kutokana na ujitokezaji wao katika taswira mbalimbali. Anaendelea kueleza kuwa baadhi yao wamemtazama mwanamke kama mfungwa anayewekwa ndani muda wote pasipo kupewa ruhusa ya kutoka nje. Hali hiyo inamfanya mwanamke kukosa haki zake na uhuru wa kutembea kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Athari ya mtazamo huo ulimfanya Challigha (2011) kuwatazama wanawake kama kundi la watu ambalo limekandamizwa na kutengwa kwa muda mrefu bila kushirikishwa katika kumiliki mali. Hivyo, jitihada za dhati zinapaswa kufanyika kuhakikisha diwani iliyoandikwa na mtunzi mwanamke inapatikana ili kuweza kuhakiki mtazamo wake kuhusu nafasi ya mwanamke. Ukweli ni kuwa swala la upatikanaji wa diwani za watunzi wa kike hasa karne hii ya 21, licha ya ukuaji wa taaluma ya uandishi bado ni hafifu. Mtunzi nguli Mlokozi katika dibaji ya kitabu hiki anakiri kuwa watunzi wa mashairi wapo na wanazidi kuongezeka. Anaendelea kusema wapo watunzi wa ushairi wa kijadi ambao ni wengi, washairi wa bongo flava, na wachache wanaotunga ushairi huru au mavue. Hata hivyo, anabainisha changamoto ya uhaba wa wachapishaji wa mashairi nchini Tanzania. Hali

inayosababisha upungufu wa diwani mpya za mashairi katika fasihi ya Kiswahili. Kwa hiyo, licha ya changamoto anayoieleza, mwandishi wa diwani hii ya kurunzi ameweza kuichapisha na kutuwezesha kupata nafasi ya kuhakiki mtazamo wake juu ya maswala yanayomuhusu mwanamke.

**Historia ya Kitabu**

Kurunzi ni mkusanyiko wa kwanza wa mashairi ya Dkt. Rose Mbijima kilichoandikwa mwaka (2019) na kuchapishwa na Moccony Printing Press, Dar es Salaam. Mashairi haya kifani, yamesheheni lugha ya ishara, picha, mafumbo na hata istiara. Aidha, yana maumbo na urari wenye ubunifu. mbali na ubunifu wa kifani , mtunzi anadhihirisha ubunifu wa kififkra, anaibua mawazo mapya na kuyasuka upya mawazo ya zamani kulingana na wakati wa hadhira yake. Kimaudhui mashairi haya ni kurunzi inayomulikia masuala ya siasa, malezi, uchumi, ufisadi, ndoa, dini na hata TEHAMA. Kurunzi inaleta katika ulimwengu wa fasihi mada mpya ambazo hazijawahi kujadiliwa kwa undani na washairi wa Kiswahili.

**Mbinu na Nadharia ya Utafiti**

Makala haya yamechunguza nafasi ya mwanamke kama anavyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Makala imetokana na utafiti wa kimaktaba. Data za makala zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na uhakiki wa diwani teule. Kupitia usomaji huo, mtafiti alipata data zinazohusiana na kusudi la makala. Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika katika uteuzi wa diwani teule. Diwani ya kurunzi iliteuliwa kwa kigezo kuwa ni diwani iliyoandikwa na mtunzi mwanamke nchini Tanzania iliyoweza kuchapishwa na kutumika katika ufundishaji katika viwango mbalimbali vya elimu hasa vyuo vikuu. Mbinu hii ya usampulishaji ilitumika ili kuweza kukidhi malengo ya makala haya. Mtafiti aliisoma diwani teule ya *Kurunzi,* kisha kunukuu mafunuo juu ya mwanamke, yaliyofuniliwa ili kuyafanyia uchambuzi na uhakiki. Katika makala haya, data zimechambuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mchakato wa Uchambuzi ulihusisha, nukuu za mashairi yanayomfunua mwanamke ili kupata data zilizokusudiwa. Data zimechambuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya ujaala.

Nadharia ya ujaala inaongozwa na msingi mkuu wa kuamini kwamba maisha ya mwanadamu pamoja na matendo yake yote vinatawaliwa na kuongozwa na nguvu za Mungu (Jaala) wake (Wamitila, 2002). Wanaujaala wanaamini kuwa kila mwanadamu anaweza kutenda jambo lolote kwa kuongozwa na mwenyezi Mungu kama mpaji wa nguvu na uwezo. Naye, Ponera (2014) anashadidia hoja hii kwa kusema kuwa nadharia ya Ujaala hujinasibisha na dini ya mwanadamu ambapo anaamini utendaji wake wa mambo yote maishani mwake hutegemea uwezo wa Jaala (Mungu). Mtazamo wa wanaujaala unachochea imani kwa wanawake kuwa uwezo waliopewa wanaume katika kufanikisha mambo mbalimbali basi mungu huyo huweza kuwapatia kisha wakatenda sawa au zaidi ya wanaume.

**Matokeo ya Utafiti na Mjadala**

Data za makala haya zinaonesha kuwa, mwanamke amefuniliwa katika mitazamo miwili muhimu. Kwanza, mwanamke amefuniliwa kitamaduni na pili, mwanamke amefunuliwa kisasa. Mwandishi Rodney (1972) katika kueleza mtazamo kuhusu jinsi, anasema kuwa majukumu kwa wanajamii katika jamii nyingi ulimwenguni hasa za Kiafrika zimegawanywa kufuatia uana na pia kwa kutumia utamaduni wa jamii husika. Anaendelea kueleza kuwa, wakati au kipindi cha historia pia huwa na mchango katika kugawanya majukumu. Data zilizopatikana katika kitabu cha Kurunzi zimetumika katika kuonesha namna mwanamke alivyofunuliwa katika vipindi hivi viwili vya kimapokeo na kisasa. Makala haya yanakitazama kipindi cha kimapokeo kama kipindi kilichokuwapo kabla ya karne ya 20 na kipindi cha usasa kuanzia karne ya 20 hadi sasa. Aidha, data zinaonesha kuwa mwanamke ni mtu ambaye huweza kuvaa uhusika zaidi ya kuwa mama na mke nyumbani ambaye uwezo wake wa kiutendaji umefungwa ndani ya mipaka na matakwa ya mme wake. Makala haya yanafafanua mafunuo juu ya jinsi ya kike ilivyotazamwa kwa kuzingatia vipindi vyote viwili kwa kutazama mafunuo chanya na hasi.

***Mtazamo wa Kimapokeo kuhusu Mwanamke***

Baada ya uchanganuzi wa data uliofanyika, matokeo yanaonesha kuwa mwanamke katika diwani ya kurunzi amefunuliwa katika mtazamo wa kimapokeo katika nyanja mbalimbali. Mtazamo wa

kimapokeo ni ule wa kitamaduni katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji yanayomuhusu mwanamke. Mafunuo ya kitamaduni ni yale yanayomtazama mwanamke kwa kuzingatia misingi ya jamii iliyomkuza mtunzi wa diwani hii. Mwandishi kama wanawake wengine katika jamii yake anaonesha katika kazi yake kuwa yapo mambo mbalimbali ya msingi ambayo mwanamke hana budi kuyafanya bila kujali kiwango cha ustaarabu alichokifikia kutokana na maendeleo yaliyopo katika jamii. Hivyo, data za makala haya kutoka kataka diwani hii ya Kurunzi, zinabainisha mambo ya kimapokeo ambayo bado yanamashiko katika jamii ya sasa yanayompasa mwanamke kuyatenda.

Mtunzi katika shairi la ***"wasikilize"*** anatueleza nasaha anazopewewa kichuna na mme wake. Mwandishi anatumia jina kichuna kumrejelea mwanamke kutoka kijijini na kuletwa mjini kama mke. Jambo hili la kutafuta mke linaonesha kuwa huwenda mtazamo wa jamii nyingi za kiafrika kuwa ukitaka kuoa ni vyema kurejea nyumbani bado lina mashiko katika jamii zetu. Katika ubeti wa tano mwandishi anasema

Mabonde nimevuka, mito nimeongelea,
Kwa uhodari mkubwa, milima nikaipanda,
Sifa wakanisifia, kila jina nikaitwa,
Tega sikio kichuna, tuliza wangu mtima.

Katika ubeti huo mwanaume anaeleza namna ilivyo mgharimu katika jitihada zake za kumtafuta mwanamke wa maisha yake. Ubeti huu unadhihirisha wazi kuwa mwanamke ni mtu ambaye hutafutwa sehemu yoyote na mwanaume anapohitaji kuoa. Jambo hili, linadhihirisha kuwa mwanaume ndiye mwenye uchaguzi na maamuzi ya kupenda na kisha kuoa na si mwanamke. Utamaduni huu umeendelea kuenziwa katika jamii nyingi, hali inayosababisha wanawake wengi kuwa waoga kueleza hisia zao wakati wanapompenda mwanaume na kuhitaji kuolewa naye. Hivyo, kusubiri majaliwa ya mwenyenzi Mungu juu ya kile atakachoamua juu ya maisha yao kama inavyoelezwa katika nadharia ya ujaala.

Pia, data zinaonesha, kupitia muhusika mwanaume, anafunua nafasi nyingine ya mwanamke kama mlezi bora wa familia. Lengo la mwanaume kuoa ni kuhakikisha anampata si mwanamke tu, bali mwanamke ambaye atakuwa mama bora kwa familia yake. Katika ubeti wa tisa anamueleza kichuna wake maneno haya;

Lea yako familia, imarisha yako nyumba,
Yasafishe mazingira, wakuite mama bora,
Kuwa ruwaza kichuna, milele nitakupenda,
Tega sikio kichuna, tuliza wangu mtima.

Ubeti huu umejaa nasaha na ahadi kutoka kwa mwanaume kwenda kwa kichuna. Maneno haya yanaonesha wajibu kwa mwanamke kuwa anayo kazi ya kuhakikisha anakuwa mfano bora wa kuigwa katika jamii, kwa kutekeleza wajibu wake wa kulea familia yake. Majukumu hayo yanapofanywa kwa ufasaha humfikisha mwanaume katika kilele cha furaha na matamanio yake ya kuwa na mke bora. Hivyo, humlipa upendo kama tunu kwa kufanikisha furaha yake, jambo ambalo kwa hakika linamuondoa mwanamke katika nafasi ya kufanya vitu kwa utashi wake bali kwa ajili ya heshima ya mwanaume.

Vile vile, mwanamke anaendelea kufunuliwa kama mshauri wa watoto katika familia. Jukumu hili muhimu tangu enzi linaonekana kutekelezwa na wanawake katika jamii. Jamii inatazama tabia njema za watoto au vijana hutokana na wanawake kutimiza majukumu yao ipasavyo na kiyume chake. Mtunzi anaikumbusha jamii inayozungumzia usawa wa kijinsia katika nyanja zote kuwa wajibu wa kutoa ushauri ni jukumu muhimu linaloelekezwa kwa akina mama. Mtunzi anaeleza katika shairi la *"mgogoyo"* kuwa;

Mwanangu nakuusia, usinitoe manani,
Acha kupuyanga puyanga, chuo sawa na bahari,
Sifa zake wazijua, itakumeza bahari,
Mwanangu nakuusia, usinitoe manani.

Katika ubeti huu unadhihirisha mtazamo wa kimapokeo kuwa ushauri na nasaha za wazazi hasa mama ni kitu muhimu katika mafanikio ya mtu yeyote. Mwanadishi anaonesha msisitizo wa mzazi katika mshororo wa kwanza na wa mwisho katika ubeti huo juu ya hofu yake kwa mwanae. Mama kama mzazi anatamani mwanaye akumbuke na kuhakikisha kuwa ushauri anaompatia haumtoki kamwe katika moyo wake. Mtunzi anaikumbusha jamii kuwa swala la kutoa nasaha njema na makatazo ni endelevu kwa wanawake wa zama zote. Pia, halina mipaka wala ukomo wa kutolewa, mathalani mtunzi anamtumia kijana ambaye yuko katika umri wa kuanza chuo kama mfano kuwa ushauri na nasaha za wazazi hazina ukomo.

Pia, Mwandishi katika shairi la "asante mama" anapigilia msumari wa kimapokeo kuwa mama ndiye mtu wa thamani sana dunia. Mtunzi anatukumbusha hilo pale anapotoa shukrani zake kwa mama yake kwa malezi bora ambayo kwa hakika hawezi kuyalipa. Mtunzi anaonesha kuwa mama katika kutimiza wajibu wake wa malezi kuna nyakati ambazo alilala bila kula, alikesha wimawima na hata mwili wake kugeuzwa kuwa msala. Mambo haya kama yalivyooneshwa na mtunzi yanaweza kufanywa na mama pekee. Mtunzi katika ubeti wa tano anaonesha ukubwa wa nafasi ya mama katika malezi anasema;

Hata nijenge ghorofa, Kilimanjaro mlima,
au nikupe dunia, pande zote kutawala,
Haviwezi thaminika, ulotenda kufikiwa,
Nikulipe nini mama? Sinacho cha kukulipa!

Katika ubeti huo wa tano ni dhahiri kuwa mwanamke amepewa nafasi ya juu sana kwa sababu ya kutimiza wajibu wake wa kimalezi kwa watoto wake. Mtazamo huu umeendelea kudumu kwa muda mrefu sasa lakini unajenga ubaguzi hasa kwa wazazi wa jinsia ya kiume. Maelezo ya mshairi hayadhihirishi nafasi ya mwanaume (baba) katika malezi kabisa licha ya kuwa jitihada nyingi zinafanywa naye kuhakikisha ustawi wa familia yake. Hivyo, mwanamke na mwanaume wote wana uwezo sawa wa kimalezi kwani mpaji ni kwa Mungu, watakaposhirikiana kwa pamoja jamii itakuwa na watu bora waliopata malezi bora kutoka kwa wazazi wote.

***Mtazamo Hasi wa Kimapokeo Kuhusu Mwanamke***

Makala haya yamebaini kuwa mwanamke amefunuliwa kwa sifa hasi ambazo zimeonekana tangu zama za mapokeo. Data zinathibitisha kuwa mwanamke bado anakabiliwa na sifa mbaya katika jamii kama chanzo cha uovu kama inavyojidhihirisha katika diwani yake. Kupitia shairi la "mgogoyo" mwanamke amechorwa kama kiumbe mlaghai ambaye anahatarisha usalama na mafanikio ya kimasomo ya mwanaume. Mtunzi anaonesha jinsi mzazi akimuasa mwanae katika safari yake ya masomo ya chuo kikuu anasema.

Ogopa ukajitenge, jiepushe na nisai,
Watakurudisha nyuma, kimasomo na kiuchumi,
Bahari itakumeza, ukavuliwa ma'nani,
Mwanangu nakuhusia, usinitoe maanani.

Katika ubeti huu mwanamke anaumbiwa sifa ya kutisha, kwamba mwanamke ni kiumbe cha kuogopa kukutana nacho ikiwa atahitaji kufanikiwa katika taaluma na uchumi. Mwanamke anaumbiwa sifa ya ufilisi wa fedha za mwanaume. Hivyo rai ya mtunzi ni kuwa ikiwa mwanaume atahitaji kufanikiwa anapaswa kujiweka mbali na mwanamke. Mtazamo huu unaonekana kumpaka mwanamke sura mbaya katika jamii licha ya ukweli kuwa wapo wanawake wanaolenga kupata fedha kutoka kwa wanaume. Hata hivyo hawaondoi sifa ya uwapo wa wanawake wema ambao ni msaada kwa wanaume katika maswala ya kiuchimi na elimu.

**Mwanamke kama Chanzo cha Uonevu Dhidi ya Jinsi Yake**

Mtunzi katika shairi la mtetezi wao anamfunua mwanamke kama chanzo cha ukatili dhidi ya watu wengine wa jinsi yake. Mtunzi anasimama kama mama na mlezi wa familia kukemea kwa dhati tabia zinazofanywa na wanawake dhidi ya wafanyakazi katika nyumba zao. Mwandishi anaonesha kuwa wanawake wenyewe ndio sababu ya kukatisha ndoto za kielimu za wasichana wengi kwa kuwaleta mjini kufanya kazi za ndani kama anavyosema katika ubeti wa pili.

Vijijini kuwatoa, mjini tunawaleta,
Ahadi kuwamwagia, pesa nene watalipwa,
Shuleni kuwaipua, kwa ushawishi mkubwa,
Sisi ni chanzo cha yote, tubadilike tabia.

Ubeti huo, unaeleza namna mwanamke anavyokatili maendeleo ya mwanamke mwenzake. Wanawake wamekuwa vinara wa ushawishi kwa kuwaachisha masomo wasichana wenye umri mdogo kutoka maeneo mbalimbali ya vijijini na kuwaleta mjini kufanya kazi za ndani. Kama anavyoeleza maisha magumu ya vijijini ni chanzo kikuu cha kufanikisha urubuni unaofanywa na wanawake hao. Hivyo, mabinti wadogo wanashawishika kwa fedha wanazoahidiwa kuja kupewa mjini, hali inayosababisha kukatisha ndoto zao za kielimu.

Aidha, mwanamke anaonekana katili zaidi kwa kufanya udhalilishaji na kuvunja haki za binadamu kwa wasichana wanaowaleta mjini. Mtunzi katika ubeti wa nne anasema kuwa

Mjini wakifikishwa, mitaji wanageuzwa,
Wanaume kutafutiwa, kwafedha kuwanunua,
Pasi huruma twatenda, uliokithiri unyama,
Sisi ni chanzo cha yote, tubadilike tabia.

Ubeti huu mtunzi anakemea tabia mbaya na ya kikatili ya kuwageuza wasichana wadogo kuwa kitega uchumi. Jambo hili sijema kulisikia likitendwa na wanawake ambao wamepabwa kwa sifa ya umama, walezi wa familia na kioo cha nyumba kama alivyojieleza katika ubeti wa kwanza wa shairi hili. Wanawake wanaotekeleza shughuli hizi za kikatili na kidhalilishaji katika jamii hawafai kuigwa katika jamii. Matendo haya yanadhihirisha kuwa adui wa mwanamke ni mwanamke mwenzake aliyekosa utu.

Sambamba na hayo, mwanamke anaonekana kiumbe asiye na upendo wala kujali. Katika shairi hili ubeti wa nne hadi saba, mtunzi anaonesha tabia za kutojali na zisizodhihirisha upendo kabisa kwa wafanyakazi zinazofanywa na wanawake. Mtunzi anasema wafanyakazi wamekuwa wakifanyishwa kazi bila kupata muda wa kupumzika, wanageuzwa kuwa ombaomba barabarani, wanashinda bila kula licha ya kazi ngumu wanazofanya. Mwandishi katika ubeti wa sita anasema

Tumegeuka wanyama, tukiwatesa mayaya,
Mishahara kutowapa, hatuwalipi kwa muda,
Miezi miwili mpaka, miezi juu ya sita,
Sisi ni chanzo cha yote, tubadilike tabia.

Mtunzi katika ubeti huo anatuonesha namna wanawake walivyo chanzo cha ukatili dhidi ya wanawake wenzake. Licha ya mambo yote wafanyakazi wanayotendewa kama yalivyoelezwa bado wanashindwa kulipwa hata stahiki zao kwa wakati. Tabia hizi ni mbaya kutekelezwa na mwanamke ambaye ni mfano wa kuigwa na mjenzi wa jamii yenye kujali haki, upendo na usawa kwa kila mtu. Usawiri huu wa mwanamke unadhihirisha kuwa uwezo alionao mwanaume wa kutenda matendo mema au maovu, unapatikana pia hata kwa wanawake katika jamii.

### *Mtazamo wa Usasa Kuhusu Mwanamke*

Katika mtazamo wa usasa mtunzi wa diwani ya kurunzi, amemfunua mwanamke kwa mtazamo mpya zaidi ukilinganisha na ule wa kimapokeo. Data zinaonesha kuwa mwanamke ameongezewa uwezo katika Nyanja mbalimbali za maisha yake na mahusiano yake na jamii inayomzunguka. Mtunzi amemfunua mwanamke katika utekelezaji wa majukumu kadha wa kadha kama ilivyobainishawa.

#### *Mwanamke kama Mwanamapinduzi*

Mwanamapinduzi ni mtu ambaye huleta mageuzi au mapinduzi katika Nyanja mbalimbali za maisha yanayomzunguka. Katika shairi la "maisha ya ndoa" mtunzi anamfunua mwanamke katika mtazamo wa kimapindunzi ambaye anapinga mfumo dume katika ndoa. Mwanamke anauvunja ukimya wa muda mrefu wa kukubali na kutii kila kitu kutoka kwa mume. Mwanamke anajaribu kumuweka wazi

jinsi vile mwanamke wa kisasa anavyowaza na kuhitaji kutendewa katika maisha ya ndoa. Mwanamke katika ubeti wanne anamueleza mme wake kuwa.

Mme tega masikio, nisikilize kwa makini,
Majukumu nayajua, jikoni hadi chumbani,
Kuchapana zilipendwa, ndoa sio utumwa,
Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?

Katika ubeti huu mwanamake anatoa rai kwa mme wake, akimtahadharisha kuhusu mienendo ya kimazoea ya kuwapiga wanawake na kuwatumikisha katika ndoa kama watumwa. Hivyo anaamua kupaza sauti na kupinga vikali swala la kupigana katika ndoa kwa sasa. Aidha, anashangaa watu wengine ambao wanaoishi katika maisha ya kale ya kukubali utumwa ndani ya ndoa kama anavyoeleza katika mshororo wanne wa ubeti. Swala la ndoa kwa sasa katika jamii yetu hasa karne ya 21, linapinga na kukemea maswala yote yanayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia katika ndoa. Wanawake kwa wanaume wanasimama kidete kupinga na kuchukua hatua dhidi ya wale wote wanaotekeleza vitendo hivyo vya kikatili. Mathalani katika nchi ya Tanzania, madawati mengi ya jinsia yamefunguliwa kila sehemu ya nchi kwa lengo la kuhakikisha ukatili na unyanyasaji wa wanawake unakomeshwa.

Aidha, mtunzi katika shiari hili anakwenda mbele zaidi kwa kumtumia mhusika mke kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusu matamanio ya kile wanawake wanachokitaka katika ndoa. Katia ubeti nane (8) hadi wa kumi (10) katika shairi hili, yanatajwa mambo ambayo mwanamke anatamani yafanyike katika ndoa. Kwanza, mwanamke anahitaji kusaidiwa majukumu kama vile kuchota maji, kutamsaidia mwanamke kuwa mtulivu na mwenye kujituliza nyumbani. Pili, mwanamke anahitaji kupetiwa petipeti kama navyoeleza katika ubeti wa tisa, mshororo wa kwanza na pili

Mwanamke ndege njiwa, apetiwe peti peti,
Asiguswe kwa mabaya, atapeperuka mbali.

Mtunzi anachoeleza hapa ni kuwa mwanamke anahitaji maneno laini, na kukingwa na hatari zote kutoka ndani. Mwanamke hufananishwa na njiwa huruka kwenda mbali pindi anapokabiliwa na hali hatarishi nyumbani. Mwanamke huyu anapaza sauti juu ya mapinduzi ndani ya nyumba ili kuhakikisha ndoa zinakuwa bora na salama kwa kila mtu kuweza kuishi kwa amani. Aidha katika ubeti wa kumi mwanamke anapaza sauti juu ya mfumo dume katika ndoa pale anasema.

Wanaume mwachekesha, madaraka punguzeni,
Uwapo nyumbani pika, ndoa zipalilieni,
Saa zipi nitapika, mimi wewe tu kazini?
Haya maisha ya ndoa, wenzangu mnaishije?

Katika ubeti huu mwanamke anahitaji usawa katika utekelezaji wa majukumu nyumbani. Katika karne hii ambayo mwanaume na mwanamke wanahaki sawa katika ajira, ni muhimu kusaidiana kwani wote wanakuwa kazini. Jambo hili ambalo analieleza ni ishara ya kimapinduzi kwa mfumo uliozoeleka katika jamii nyingi za kiafrika. Bila kujali kiwango cha elimu na ustaarabu ambao mtu binafsi ameufikia, mtazamo wa jamii ni kuwa shughuli nyingi za nyumbani hasa kupika ni jukumu la mwanamke. Hivyo, kupinga swala hili hadharani ni kudhihirisha kuwa wanawake katika karne hii ya 21 wanahitaji usawa na usaidizi katika mambo mbalimbali ambayo awali jamii iliyaelekeza kwa mwanamke, bila kujali majukumu yake mengine aliyobebeshwa na jamii yake. Mapindizi haya yanaashiria kuwa mwanamke anatamani usawa katika utendaji, kwani Mungu amewapatia nguvu na uweza wa kutenda sawa kama binadamu.

Pia, katika shari la *"nisai"* mwanamke anadhihirisha mtazamo mpya wa kimapinduzi juu ya swala la elimu kwa wanawake. Mwanamke anahitaji kupewa haki ya kupata elimu kama ilivyo kwa wanaume. Swala la ujinsi sio sababu ya kumzui mwanamke kupata elimu kama anavyoeleza katika ubeti wa tatu.

Elimu wajibu wetu, awali hadi vyuo,
Jinsi sio ulemavu, wakitufungia ndani,

Tusimame mnadabu, peke yetu twatosheni,

Nisai sote muhimu, wagombezi wa jamii.

Katika ubeti huo wa tatu mtunzi anatumia neno nisai kurejelea wanawake. Wanawake wanahitaji kujisimamia wenyewe kuhakikisha kuwa wanapambana ili kuhakikisha wanapata elimu bora kuanzia msingi hadi vyuo. Aidha, mtunzi anakumbusha kuwa jinsi sio ulemavu kama ilivyo kuwa ikitazamwa kimapokeo kuwa wanamke hapaswi kupewa elimu. Jamii ya sasa inapaswa kutambua kuwa elimu ni wajibu na haki ya msingi kwa wanawake wote kwa viwango vyote. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha wanawake wote wanaungana kuhakikisha jambo hili linafanikiwa.Ikizingatiwa kuwa mwanamke na mwanaume wamepewa uwezo sawa wa kutenda kutoka kwa mwenyezi Mungu.

Aidha, mwanamke anahitaji kufanya mapinduzi katika swala zima la uongozi. Katika jamii zetu ilizoeleka kuwa mwanamme ndiye mwenye nafasi kubwa ya kufanya maamuzi na kuongoza kuanzia kiwango cha familia hadi ngazi ya nchi kama anavyoeleza katika ubeti wa tisa.

Walikufanya bahau, ukageuzwa mlinzi,

Nawe ukawa mtuvu, kunguru kwako hodari,

Wakakuita ubavu, hufai madarakani,

Nisai sote muhimu, wagombozi wa jamii.

Mwanamke anawaeleza wenzake umuhimu wa kufanya mapinduzi ya kiuongozi kwa kuondokana na mitazamo iliyokuwapo ya kumfanya mwanamke kuwa mlinzi wa nyumba. Pia kuwa msaidizi tu kwa sababu yeye ni ubavu wa mwanaume, hivyo hafai kuwa madarakani bali kumsaidia mwanaume katika kutekeleza shughuli zote za kiutawala alizonazo mwanaume. Hivyo, mwanamke anatoa wito katika ubeti wa kumi (10) wa shairi la "nisai" akiwataka wanawake kufanya jitihada kuhakikisha wanashika hatamu za kiuongozi kama anavyosema.

Nasi tushike hatamu, tuwemo uongozini

Tusiwe wapendelevu, kuendekeza nafsi

Ni bora tuwe hashimu, walafi wasweke ndani,

Nisai sote muhimu, waombozi wa jamii.

Katika ubeti wa kumi wanawake wanahamasishwa kushika hatamu mbalimbali za uongozi katika jamii. Wanamwake wanapaswa kuepeuka tamaa binafsi ili waweze kuwa viongozi bora na pia kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao wa kulinda rasilimali za nchi na kuhakikisha walafi wanasweke ndani. Hakika mtazamo huu unadhihirisha dhamira ya kweli ya kimapinduzi waliyonayo wanawake wa kisasa kuhusu haki yao ya kuwa viongozi na kufanya maamuzi sawa na yale wanayofanya viongozi wanaume.

**Hitimisho**

Makala haya yalilenga kubainisha mtazamo wa mtunzi mwanamke wa diwani, dhidi ya sifa anazomfunua nazo mhusika mwanamke katika kazi yake. Mtunzi wa diwani hii ya kurunzi amejitabanaisha wazi kuwa maswala yanayomuhusu mwanamke yanaweza kujadiliwa kimapokeo na kisasa pia. Data zimeonesha kuwa zipo sifa mbalimbali za kimapokeo alizopewa mwanamke zinazofaa kuendelezwa kama vile kuwa mama bora wa familia, mshauri na mlezi wa familia. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa mtunzi wa diwani ya *Kurunzi,* ameonesha nafasi ya mabadiliko ya jamii kuhusu mtazamo wa wajibu wa mwanamke wa kisasa katika utendaji wake. Mwanamke wa kisasa amefunuliwa na mtunzi kama mwanamapinduzi katika kutaka usawa katika nyaja mbalimbali za kijamii kama ndoa, elimu na uongozi. Hata hivyo, mtunzi hakuona haya kuonesha udhaifu wa mwanamke licha ya kuwa yeye ni mwanamke. Mtunzi amekemea tabia mbaya na matendo maovu yanayotendwa na wanawake katika jamii. Mtunzi anamfunua mwanamke kama chanzo cha uovu katika jamii na pia sababu ya kukwamisha maendeleo ya jinsi yake katika nyanja mbalimbali za maisha. Matokeo haya yanatuonesha kuwa mwanamke si tu anachorwa katika nafasi hasi na watunzi au wahakiki wa kiume pekee, bali hata mtunzi mwanamke anaweza kufanya hivyo pia. Aidha, ni dhahiri kuwa mtazamo wa kimapokeo kumuhusu mwanamke, chanya au hasi wote unasadifu hali ya kumtweza mwanamke kwa kumuonesha kama kiumbe duni na katili katika jamii.

**Marejeleo**

Challigha, N. E. (2011). *Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia katika Fasihi Picha ya Katuni Mnato za Kiswahili*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Indede, F. (2011). Mwanamke Angali Tata Katika Ushairi wa Kisasa? *Swahili Forum, 18,* 163-197.

Lyatuu, J. (2011). *Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na Kiume: Uchaguzi katika Riwaya Teule*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mbijima, R. (2019). *Kurunzi*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mwakanjuki, N. (2022). Mapungufu ya Kiutamaduni Yanavyoathiri Ustawi wa Mwanamke katika Jamii: Mifano Kutoka Riwaya ya *Sikujua*. *Jarida la Fahari ya Kiswahili, 1(1),* 115-130.

Ngaiza, M. K. (2004). Harmonization and Mainstreaming Gender in Local Government or Transforming Patriarchy*:* The Case of Two Wards in Bukoba District Council, Tanzania. *Tanzanian Journal of Development Studies, 5,* 25-38.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi.* Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Rodney, W. (1972). *How Europe Underdeveloped Africa.* London: Rogle-L'Ouverture Publishers.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Open University Press.